



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO



TANGAZO KWA TAASISI ZA UMMA:

KUZINGATIA SHERIA YA SERIKALI MTANDAO NA. 10 YA MWAKA 2019

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) inazikumbusha Taasisi zote za Umma, kuwasiliana na Mamlaka ya Serikali Mtandao kabla ya kuanzisha au kujenga Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA, ili kujenga ufanisi na kuleta uwiano wa kutoa huduma kwa umma kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 24 cha **Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019**.

Sheria ya Serikali Mtandao, imeipa Mamlaka jukumu la kutoa ushauri wa namna wa utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya TEHAMA pamoja na kuruhusu kuendelea kwa Miradi hiyo, ikiwa ni pamoja na kuzitaka Taasisi husika kutoa Taarifa za utekelezaji mara kwa mara pamoja na taarifa ya mwisho baada ya kukamilika kwa Miradi hiyo. Aidha, Mamlaka inalo jukumu la kutoa katazo la kutoendelea kwa Mradi wowote wa TEHAMA endapo utabainika kutokuwa na tija kwa Taifa.

Vilevile, Sheria hii inazitaka Taasisi zote za Umma zinazohusika na ujenzi wa Miundombinu ya Serikali ikiwemo Barabara, Reli na Majengo kuhakikisha inawekewa mazingira wezeshi kwa ajili ya kupitisha Miundombinu ya

TEHAMA kuanzia wakati wa kuandaa michoro ya ujenzi wa Miundombinu hiyo ikiwa ni matakwa ya **Kifungu cha 23 (2) cha Sheria hii**.

Ukiukwaji wa Sheria hii ni kosa la Jinai na adhabu yake ni kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili lakini isiyozidi **shilingi milioni ishirini au kifungu cha muda usiopungua miezi sita Jela lakini usiozidi miaka mitano au kwa vyote viwili, kama inavyoelezwa katika vifungu na 57 na 58**. Taasisi za Umma zinahimizwa kuzingatia matakwa ya Sheria hii ili kuwa na Matumizi ya TEHAMA salama na yenye tija kwa Serikali.

Sheria ya Serikali Mtandao inapatikana kupitia tovuti za Mamlaka ya Serikali Mtandao (www.ega.go.tz), **Bunge, bunge.go.tz** na eGA online TV.

IMETOLEWA NA:

MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (eGA)

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz

“Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma”